HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA KIGOMA MHE. THOBIAS ANDENGENYE WAKATI WA KUWAAPISHA WAKUU WA WILAYA WAPYA TAREHE 21 JUNI 2021

UTANGULIZI

Mhe. Rashid Kassim Mchata-Katibu Tawala wa Mkoa

Ndg. Ndug. Amandus Nzamba - Mwenyekiti wa CCM Mkoa

Mhe. Col. Michael Masala Ngayalina - Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe

Mhe. Col. I. A. Mwakisu- Mkuu wa Wilaya ya Kasulu

Mhe. Col. E.M. Malasa- Mkuu wa Wilaya ya Kibondo

Mhe. A.J. Magwaza –Mkuu wa Wilaya ya Kakonko

Mhe. Ester Alexander Mahawe-Mkuu wa Wilaya Kigoma

Mhe. Hanafi Hassan Msabaha- Mkuu wa Wilaya ya Uvinza

Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi ya Mkoa

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kigoma Ujiji

Mhe. Wenyeviti wa Halmashauri za Mkoa wa Kigoma,

Wahe. Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Ndg. Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Ndg. Watendaji katika ngazi mbalimbali,

Ndg. Wageni Waalikwa,

Ndg. Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

UTANGULIZI

Kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutulinda na kutukutanisha katika hafla hii ya kuwaapisha Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya walioteuliwa kuongoza Wananchi katika Mkoa wa Kigoma. Binafsi kama Mkuu wa Mkoa pia nafurahi kuwaapisha Wakuu wa Wilaya wateule kwa Mara ya Kwanza tangu nilipoteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma.

Pia nipende kuwakaribisha sana katika Mkoa wa Kigoma Mkoa wenye watu wachapakazi, wanaojituma na wapenda maendeleo, Mkoa uliobarikiwa kuwa na ardhi yenye rutuba na mvua za kutosha pamoja na hali ya hewa nzuri, ni Mkoa pekee uliopo kimkakati ambao upo katika jumuiya mbili za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya baada ya ukaribisho huo basi name nitumie muda kidogo kuawapitisha katika yale ambayo tunapaswa kwenda kuyasimamia na kutekeleza katika dhamana tuliyopewa na Kiongozi wetu Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Maelekezo haya ni nia ya kuwapa taarifa za awali Wah. Wakuu wa Wilaya kuhusu hali ilivyo katika Wilaya zenu na mambo ya msingi wanayopaswa kuanza nayo katika kipindi hiki. Maelekezo haya yamejumuisha Maagizo yaliyotolewa na Viongozi mbalimbali wa Kitaifa ambayo utekelezaji wake ni wa kila siku.

Aidha, katika maelekezo haya pia nitakuwa nagusia maagizo mbalimbali yanayotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yaliyotolewa kupitia Waraka Na. 13 wa tarehe 23 Desemba, 2015 wenye Kumb.Na. CAB.110/156/01”B”/11 na memngine mengi ambayo yameendelea kutolewa kwa nyakati tofautitofauti.

SUALA LA ULINZI NA USALAMA

Katika Wilaya zetu tuendelee kusimamia suala la ulinzi na usalama. Vikao vya Kamati za Ulinzi na Usalama katika ngazi za Vijiji na Kata havina uratibu mzuri katika baadhi ya maeneo. Wakuu wa Wilaya mnayo dhamana kubwa ya kuhakikisha Vikao hivyo vinaratibiwa vizuri na pale ambapo Kamati zinaonekana kutokuwa hai basi jitihada za kuzifufua zifanyike lengo ikiwa ni kuimarisha Ulinzi na Usalama kwa Wananchi wetu.

Maeneo mengi ya mipaka ya Kimataifa kwa Mkoa wa Kigoma yamekuwa yakitumia kama vipenyo kwa wageni wasiotaka kufuata Sheria. Miongoni mwa athari za wazi ni kuwepo kwa Wahamiaji haramu ambao huingia kuptia njia hizo zisizo rasmi.

Wakuu wa Wilaya kashirikianeni na Kamati za Usalama za Wilaya kuweka udhibiti katika vipenyo vyote vilivyo katika maeneo mbalimbali ili wahamiaji haramu waweze kudhibitiwa ipasavyo.

Kwa Wilaya zenye wakimbizi walio makambini kuhakikisha hawatoki kwenye makambi yao bila sababu za msingi. Wakuu wa Wilaya mkashirikiane na Idara ya Uhamiaji kudhibiti Wahamiaji haramu.

MAPATO YA HALMASHAURI

Ripoti Kuu ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo pamoja na mambo mengine imeonesha kuwa katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2020, sita (6) kati ya katika Mkoa wa Kigoma zilipata hati zenye mashaka.Hivyo mnalo jukumu kubwa la kwenda kusimamia matumizi ya fedha za Serikali, utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maedeleo.

Nendeni mkasimamie na kuhimiza Halmashauri kufanya tathmini ya kina ya uwezo wa vyanzo vyake vya mapato na ziweke mikakati

inayotekelezeka ya kuhamasisha, kuimarisha na kuboresha usimamizi wa mapato ili kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Ni vyema Halmashauri zikahimizwa kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuondokana na utegemezi kutoka ushuru wa mazao. Chanzo ambacho licha ya kuwa ndicho kikuu lakini hakiaminiki kwa kuwa kinategemea sana hali ya hewa.

Wakuu wa Wilaya wasisitize matumizi sahihi ya Mashine za Kielektroniki za kukusanyia mapato (POS) ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi yake na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa mawakala/wakusanya mapato ili kudhibiti udanganyifu unaoweza kujitokeza, ikiwa pamoja na kuwasilisha makusanyo kwa muda na siyo mkusanyaji kubakia na fedha za Serikali kwenye mikono yake kama ilivyokuwa kwa baadhi ya maeneo.

HALI YA MAENDELEO NA CHANGAMOTO ZILIZOPO KISEKTA

Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tawala za Mikoa (Sura 97) kinampa Mkuu wa Wilaya Majukumu ya **Kuziwezesha na Kuzijengea Mazingira Mazuri Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopo ndani ya eneo lake ili ziweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo**. Wakuu wa Wilaya tumieni vizuri Mamlaka mliyonayo ili kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza Majukumu yake.

- Wakuu wa Wilaya nendeni mkajenge mahusiano mazuri katika sehemu zenu za kazi, Taasisi zinazowazunguka na Wananchi wote kwa ujumla. Mkumbuke kuwa majukumu mnayotekeleza yanagusa maisha na maendeleo ya Wananchi.

- Katika kuwatumikia Wananchi mkazingatie Sheria, Kanuni na Taratibu katika Utekelezaji wa Majukumu yenu. Ni utovu wa Maadili na ni uvunjaji wa Sheria kwa Viongozi na Watumishi wa Umma kutumia nafasi na Madaraka yao kujipatia Mikataba na Zabuni mbalimbali ni makosa pia kwa Viongozi na Watendaji kutumia vibaya fedha na mali nyingine za Serikali nendeni mkalisimamie hili.

- Msiende kukaa ofisini pandeni ratiba za kuwatembelea na kuwasikiliza Wananchi kujua shida, kero zao na kuzifanyia kazi, ni muhimu sana kushiriki Mikutano Mikuu ya Vijiji, Kamati za Maendeleo za Kata (WDCs), Mabaraza ya Kata na Kamati za Ushauri za Wilaya (DCC) inafanyika. Iwapo Mikutano hiyo itafanyika kwa kuzingatia ratiba zake (na pale inapobidi kwa dharura) changamoto mbalimbali zinazowakabili Wananchi katika maeneo yenu zitapatiwa ufumbuzi.

- Tengeni muda wa kusikiliza kero za Wananchi na kuzipatia ufumbuzi. Katika siku watakazotenga kwa wiki wakae na Wataalamu wa Sekta muhimu (Sheria, Ardhi, Afya, Maliasili/Misitu na Utawala) ili kupata

maelezo na ushauri wa kina utakaopelekea kupatikana kwa ufumbuzi wa kero/malalamiko wattakayopokea.

- Taarifa za Ukaguzi wa Miradi zijadiliwe na pale itakapobainika kuwepo kwa dosari, hatua za haraka za kinidhamu na kisheria zichukuliwe kwa wahusika. Nakala za taarifa hizo ziwasilishwe Ofisini kwangu.

- Simamieni ubora na viwango katika Miradi inayotekelezwa kwenye Wilaya zao na wawakemee Watendaji wasiozingatia ubora katika usimamizi wa Miradi inayotekelezwa na pale inapobidi Mamlaka zishauriwe kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma.

KILIMO

Shughuli kuu za kiuchumi katika Mkoa wa Kigoma zimejikita katika Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, Biashara na Viwanda vidogo. Kilimo kwa kiasi kikubwa kinaendeshwa kwa jembe la mkono na matumizi hafifu ya pembejeo. Kwa ujumla tija ni ndogo.

- Wakuu wa Wilaya hamasisheni matumizi ya pembejeo na zana bora za kilimo na wasimamieni kwa karibu Maafisa Ugani pamoja na Wataalamu wengine ili kuhakikisha kuwa wanawafikia Wananchi.

- Simamieni na kushirikiana na Wataalamu wa Kilimo katika Wilaya kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya kimkakati (Kahawa, Tumbaku, Pamba na Michikichi) ili kuinua kipato cha kaya, Mkoa na Taifa.

- Nendeni mkaimarishe usimamizi wa pembejeo za kilimo ili ziwafikie walengwa. Wahamasishe wafanyabiashara ili washiriki katika kusambaza pembejeo hizo kwa wakati hadi kumfikia mkulima.

- Zihimizeni Halmashauri kuweka mikakati ya kuwa na Matrekta kama nyenzo ya kurahisisha kilimo na kuondokana na kilimo cha jembe la mkono. Halmashauri zinaweza kuanzisha vituo vya matrekta karibu na maeneo ya uzalishaji.

- Wakuu wa Wilaya wawahamasishe Vijana waliopo Mitaani kushiriki kwenye shughuli za kilimo na kujiunga kwenye vikundi ili wapate sifa ya kukopesheka katika shughuli za kilimo.

USHIRIKA

Katika shughuli zenu nendeni mkawahimize

- wakulima na wanachama wa Vyama vya Ushirika kutumia fursa za kukopa mikopo yenye masharti nafuu katika benki zilizoanishwa na Serikali kupitia dirisha la wakulima na wadau wengine wa maendeleo ili kuimarisha mitaji yao na kuendelea kutoa huduma kwa wanachama kama ilivyotarajiwa.

- Vyama vya ushirika vya mazao na vingine kuangalia fursa ya kuanza kuwekeza katika viwanda katika Mkoa wa Kigoma kwa kutumia fursa zilizopo.

- Wananchi wengi zaidi kujiunga katika vyama vya ushirika vya mazao, Mifugo, Viwanda, Akiba na Mikopo na Vyama vya Ushirika vya aina nyingine kulingana na mahitaji ya Wananchi wa eneo husika.

MAJI

Miradi mingi haijakamilika licha ya Serikali kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kuitekeleza.

- Fanyeni ukaguzi wa miradi ya maji katika Wilaya zenu na kuainisha changamoto/vikwazo vya ukamilishaji wa miradi hiyo.

- Piteni na kujiridhisha na matumizi ya fedha zinazotolewa kugharamia miradi ya maji, mchakato wa kuwapata wakandarasi/utaratibu wa utekelezaji wa miradi husika na kuchukua hatua stahiki.

- Kakagueni na kutatua changamoto zinazokwamisha ufanisi wa Kamati na Mifuko ya Maji Vijijini.

MIFUGO

Mkoa una idadi kubwa ya mifugo katika maeneo ya msitu wa hifadhi wa Makere Kaskazini na Makere Kusini Wilayani Kasulu na katika maeneo ya Pori la Hifadhi la Moyowosi - Kigosi Wilayani Kibondo. Uwepo wa mifugo hiyo unaathiri mazingira kwa kiasi kikubwa.

- Wakuu wa Wilaya zenye mifugo ndani ya hifadhi wahakikishe wanapata taarifa sahihi za idadi ya mifugo iliyopo na athari zinazosababishwa na mifugo hiyo kwenye mazingira na vyanzo vya maji.

- Ili kupunguza migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji pamoja na uvamizi wa mapori ya akiba na hifadhi Wakuu wa Wilaya fuatilieni mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Wilaya zenu. Mipango hiyo itungiwe Sheria ndogo ili iweze kusimamiwa vizuri .

ELIMU

Changamoto:

- Upungufu mkubwa wa madawati, viti na meza, matundu ya vyoo, vyumba vya madarasa na maabara pamoja na nyumba za Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari.

- Kutokuwepo matofali ya kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi.

- Ushiriki duni wa Wananchi katika shughuli za Elimu kutokana na kutafsiri vibaya Mpango wa Elimu bila Malipo.

Maelekezo:

- Wakuu wa Wilaya washirikiane na Wadau wengine ndani na nje ya maeneo yao kufanikisha utekelezaji wa maagizo ya kutengeneza Madawati, Viti na Meza na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Elimu.

- Wananchi wahamasishwe kuendelea kutayarisha matofali na kujiwekea akiba ya kutosha/Benki ya matofali ili iwe rahisi kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ya ujenzi wa miundombinu ya Elimu.

- Wakuu wa Wilaya simamieni vizuri dhana ya Elimu ya Msingi bila Malipo na kuhakikisha hatua za kinidhamu kwa watakaokiuka maagizo ya Serikali kuhusu suala hili. *Mchango wowote unaohusu motto wa Shule(kichwa)/mzazi hauruhusiwi kabisa;* ***isipokuwa*** *pale ambapo Wananchi/wadau kupitia vikao/Mikutano yao halali wameamua kuchangia kwa nia ya kushughulikia kero fulani iliyopo katika shule yao au shule zao utaruhusiwa tu kwa kibali cha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kitakachoombwa kupitia kwa Mkuu wa Mkoa.*

- Mkaendelee kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Serikali wa kutoa Elimu bila Malipo na hamasisheni Wananchi wapeleke watoto Shule na kufuatilia maendeleo yao.

- Wakuu wa Wilaya washirikianeni na wadau mbalimbali katika ujenzi na uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu ili kukabiliana na ongezeko la Wanafunzi linaloshuhudiwa kila mwaka baada ya uamuzi wa Serikali wa kuanza kutoa Elimu bila Malipo.

AFYA

- Wakuu wa Wilaya wajiwekee utaratibu wa kufuatilia matumizi ya fedha za Ujenzi wa miundombinu ya afya kwani imebainika kuwa baadhi ya Halmashauri zimetumia vibaya fedha hizo na kuathiri ubora wa majengo yanayojengwa (hakuna *Value for Money*).

- Fuatilieni udanganyifu katika manunuzi ya dawa na vifaa tiba na wizi wa dawa na vifaa tiba ambao licha ya kubainika, hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa dhidi ya wahusika.

- Hivi karibuni nimepita katika Wilaya za Kasulu na Buhigwe kuhamasisha watu kujiunga na CHF iliyoboreshwa, bado hali ya uandikishaji wa Wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) iko chini sana. Wakuu wa Wilaya wahamasisheni Wananchi kujiunga na mfuko huo ili kuokoa gharama za matibabu. CHF iliyoboreshwa imeweka utaratibu mzuri wa matibabu ambapo sasa inaruhusu mfumo wa rufaa kutoka ngazi za chini za kutolea huduma hadi ngazi ya Mkoa tofauti na utaratibu wa zamani uliowezesha mgonjwa kupata huduma kwenye kituo kimoja kilicho karibu naye tu.

VIWANDA, BIASHARA, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

- Suala la kutenga maeneo ya uwekezaji, na kutafuta wawekezaji ni la msingi ili kufikia azma ya Serikali ya Viwanda. Kilimo kinakwenda sambamba na uchakataji wa mazao (*processing*). nendeni mkasimamie uhamasishaji wa Wananchi kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo kwa ushirikiano na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO). Shirikianeni na Shirika la SIDO litasaidia kubaini teknolojia inayoweza kutumika katika usindikaji wa mazao ya kilimo kwa mfano; michikichi na mihogo, pamoja na kupukuchua nafaka kabla ya kupeleka kwenye masokoni.

  - Katika mikutano yenu na Wananchi hamasisheni Wanawake, Vijana na Walemavu kujiunga katika vikundi ili waweze kunufaika na fedha za mikopo zinazotolewa na Halmashauri.

  - Serikali imeanza kujenda Vyuo vya VETA katika kila Wilaya, tutumie majukwaa yetu kuwahamisha wananchi wapeleke vijana VETA kujifunza utaalam katika fani mbalimbali ili waweze kujiajiri.

MALIASILI NA MAZINGIRA

- Katika kutunza mazingira Wakuu wa Wilaya wahamasisheni Wananchi kuanzisha mashamba ya miti ya kibiashara, miti ya matunda kama vile Maparachichi ya kisasa ambayo ni uchumi mkubwa sana, na ukizingatia hali ya hewa ya Mkoa wa Kigoma inaruhusu matunda hayo kustawi.
- Wakuu wa Wilaya wekeni na simamieni mikakati ya kudhibiti Uvamizi wa misitu ya hifadhi kwa ajili ya shughuli za binadamu kama kilimo cha kawaida na kilimo cha tumbaku, makazi, uvunaji wa mazao ya misitu usio endelevu na uingiaji wa makundi ya mifugo kutoka Mikoa jirani.

MPANGO WA KUDUMU WA USAFI WA MAZINGIRA

Maeneo mengi ya Miji na Vijiji ni machafu na hakuna jitihada za kuondoa taka katika maeneo hayo. Nendeni mkasimamie jitihada za usafi katika Wilaya zenu ikiwa pamoja na kutumia sheria za Mazingira za kutaka kila kaya kuwa na choo.

Kila Halmashauri iandae mikakati ya kudumu ya usafi. Ikibidi tuwe na utaratibu wa kutenga siku moja kufanya usafi kufanya usafi wa kina wa maeneo yetu.

- Uchafu wote uliokusanywa katika maeneo mbalimbali ya Manispaa na Miji uzolewe na kuhakikisha utamaduni wa kufanya usafi na kuzoa taka kupeleka kwenye madampo unadumishwa.

- Kila Mtaa uwe na sehemu maalum “vizimba” vya kukusanyia taka ili iwe rahisi kwa magari ya kuzoa taka kupita na kuchukua taka. Muhimu ni magari ya kuzoa taka kupita kila simu kuchukua taka bila kukosa ili sehemu hizo zisigeuzwe kuwa madampo ya kudumu.

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya ni matumani yangu tutaendelea kushirikiana kwa pamoja na wananchi wa Mkoa wa Kigoma katika kuweka mikakati ya kuwaletea maendeleo. Haya niliyoyasema hapa nilikuwa najaribu kuwapitisha tu kidogo mjue kazi mliyonayo ni kubwa ya kweda kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi yenye lengo la kuwaletea maendeleo Watanzania hususan wananchi wa Mkoa wa Kigoma.

Akhsanteni kwa Kunisikiliza.

==========